# Mambo matatu muhimu katika nguvu ya umma: umoja, kuweka mipango na maandamano ya amani

## THE TRIFECTA OF CIVIL RESISTANCE: UNITY, PLANNING, DISCIPLINE

**Hardy Merriman**

opendemocracy.net, November 2010
Translation: JPD Systems, December 2018

Imechapwa kwenye Jukwaa la *openDemocracy* (http://www.opendemocracy.net)

# Mambo matatu muhimu katika nguvu ya umma: umoja, kuweka mipango na maandamano ya amani

Hardy Merriman, 19 Novemba 2010

Mambo matatu yanaweza kuleta utofauti kati ya kufanikiwa na kushindwa kufanikiwa kwa mavuguvugu ya kudai haki kwa njia ya amani duniani: umoja, kuweka mipango na maandamano ya amani.

**Kuhusu Mwandishi**

Hardy Merriman alikuwa Mkurugenzi wa programu na utafiti kwenye Kituo cha Kimataifa cha Migogoro Baridi (ICNC) kuanzia 2005 hadi 2007. Alihariri kitabu kinachoitwa "Waging Nonviolent Struggle: 20th Century Practice and 21st Century Potential" (yaani Matumizi ya mapambano ya amani: Uzoefu wa karne ya 20 na umuhimu wake katika karne ya 21) kilichoandikwa na Gene Sharp, pia aliandika kwa ushirikiano kitabu kingine kinachoitwa "A Guide to Effective Nonviolent Struggle" (yaani Mwongozo wa mapambano ya dhati ya amani) .

**Nini husababisha mavuguvugu ya amani kufanikiwa?**

Tukikubaliana na usemi kwamba kwenye siasa "mtu hapewi nguvu, siku zote kupiganiwa", tunahitimisha kwamba mavuguvugu kihistoria ya kudai haki kwa amani yalifanikiwa kwa sababu, kwa kiasi fulani, yalitumia nguvu ambayo iliizidi ile ya mahasimu wao.

Hitimisho hili linakinzana na, pia linaibua maswali zaidi juu ya, dhana ya wengi kwamba nguvu huanzia kwenye udhibiti wa rasilimali vitu na uwezo wa kutumia hiyo nguvu. Kama dhana hii ingekuwa sahihi kabisa, mavuguvugu ya amani yangegonga mwamba kwa mahasimu wanaotumia mtutu wa bunduki na rasilimali za kutosha. Hata hivyo, historia inatukumbusha mavuguvugu mengi ya amani ambayo yalifanikiwa, kwa zaidi ya karne, mahasimu na vyanzo vyake vikiwa vya aina tofauti tofauti kama ubinadamu wenyewe. Hii ni mifano michache tu:

- Miaka ya 1930 na 1940, Wahindi walijipatia uhuru kwa kiasi kikubwa kwa kutoiunga mkono serikali (migomo ya kiuchumi, migomo mashuleni, migomo mitaani, kukataa kulipa kodi, kutotii sheria bila shuruti, kujihudhuru) ambavyo vilisababisha India kutotawalika na mwishowe ikawa kichocheo cha Waingereza kuondoka;

- Miaka ya 1950 and 1960, Vuguvugu la Haki za Raia nchini Marekani lilifanikiwa migomo ya kupanda mabasi ya Montgomery na kujibweteka kwenye viti virefu Nashville baada ya chakula cha mchana ambako kulizoofisha mfumo wa ubaguzi na kushawishi taifa zima kuunga mkono hiyo migomo;
- Kunzia 1965 hadi1970,Chama cha Muungano wa Wakulima kilikuwa kidogo lakini kikakua, kikianzia kwenye muungano mdogo tu usio na ufadhili wowote hadi kuonekana kitaifa kwa kupitia migomo yao ambayo ilifanikiwa sana dhidi ya mashamba ya zabibu ya California;
- Mwaka 1986 kule Ufilipino, wanaharakati walisaidiana na wanajeshi waasi katika kufanya mikutano ya upinzani kupinga udikteta wa Ferdinand Marcos uliokuwa unaungwa mkono na Marekani. Kwa kupitia maandamano ya amani, mbinu zake zote ziligonga mwamba na hivyo akaamua kuikimbia nchi;
- Mwaka 1988, Wachile waliachana na tabia ya kumwogopa dikteta hatari Augusto Pinochet kwa kumwamulia na kufanya maandamano dhidi yake. Vitendo hivyo vilififisha Pinochet kuungwa mkono kiasi kwamba hata wanajeshi wenzake wa serikali yake wakamsaliti mapambano yalipofikia kileleni, na hivyo akalazimishwa kuachia ngazi;
- Kuanzia 1980 hadi1989, Wapolandi walianzisha chama huru cha wafanyakazi kama sehemu ya vuguvugu la Mshikamano na kuirudisha nchi yao kutoka mikono ya utawala wa Soviet;
- Mwaka 1989, migomo ambayo baadaye ilijulikana kwa jina la Mapinduzi ya Amani ilipita kipindi cha mpito cha amani kutoka Ukomunisti kwenye Jamhuri ya Czechoslovakia. Hatua za namna hiyo hiyo zilizisaidia kupitia vipindi vya mpito vya amani Ujerumani Mashariki, Latvia, Lithuania, na Estonia mwaka 1991;
- Migomo, kutotii sheria bila shuruti na vikwazo vya jumuiya ya kimataifa kuanzia miaka ya 1980 vilisaidia sana kutokomeza ubaguzi wa rangi nchini Afrika Kusini mwanzoni mwa miaka ya 1990;
- Mlongo uliofuata, Waserbia (2000), Wajojia (2003), na wayukreni (2004) walitokomeza utawala wa kiimla kwa kuwakusanya watu wengi pamoja na kuzuia au kupinga matokeo ya uchaguzi ambao haukuwa wa haki na amani;
- Mwaka 2005, Walebanoni kwa kupitia maandamano makubwa ya amani walikataa majeshi ya Syria kuendelea kutawala nchi yao;
- Mwaka 2006, Wanepali waliamua kuvunja sheria na kulazimisha kurejeshwa kwa utawala wa umma;
- Kuanzia 2007 hadi 2009,wakati wa maandamano yaliyoambatana na matumizi ya nguvu na mbele ya kiongozi wa kijeshi, wanasheria wa Pakistani, makundi ya asasi za kiraia, na wananchi wa kawaida walifanikiwa kurejesha mahakama huru na kuondoa sheria za hali ya hatari.

## Wananchi wasipotii bila shuruti, watawala hawawezi kutawala

Mavuguvugu haya na mengine ya kutumia nguvu ya umma yalifanikiwa kwa sababu yaliegemea kwenye elimu ya msingi juu ya matumizi ya nguvu: kwamba karibu taasisi zote, mashirika yote na mifumo yote kwenye jamii hutegemea ridhaa, ushirikiano, na utii wa wananchi wengi wa kawaida. Hivyo basi, wananchi wakiamua kutupilia mbali ridhaa na ushirikiano wao kwa kujipanga vema kimkakati, wanaweza kutumia mabavu. Watu wasipotii bila shuruti, hapo

maraisi, mameya, wakurugenzi, majenerali, na wengine “wenye mamlaka” hawawezi kuongoza nguvu yao inakuwa imedhibitiwa.

Mbinu za kudai haki kwa amani, kama vile migomo, maandamano makubwa, kuvunja sheria, kuwa na taasisi mbadala, na ubunifu wa mamia ya mbinu nyingine, ndo zilikuwa nyenzo muhimu katika kufanikisha hili. Hazikutumika kwa sababu ya utashi, bali kwa sababu ya uhalisia zaidi kwamba zinafaa kimatendo na si kinadharia. Wengine waliotumia nguvu ya umma waliona mikakati ya hivyo ikifanikiwa kwenye nchi nyingine au kwenye historia yao, na kugundua kwamba aina hii ya upinzani ilileta mafanikio bora kuliko nyinginezo.

## Maarifa na mazingira

Hata hivyo, pamoja na munkari kupitia ushindi wa mavuguvugu ya amani, historia ya dunia ya leo inatupa mifano ya mavuguvugu ambayo hayakuzaa matunda.  Dunia ilishuhudia mapinduzi ya amani Poland na Czechoslovakia ambapo mwaka huo huo dunia ilishuhudia mauaji ya kimbari ya kwenye Uwanja wa Tiananmen. Katika mlongo wa mwisho, watu wengi walitumia njia za amani nchini Burma, Zimbabwe, Misri na Iran, lakini malengo ya mavuguvugu hayajafanikiwa hadi leo. Katika mapambano ya kujihami ambayo yalifanikiwa kule Timor ya Mashariki, nguvu ya umma ilikuwa ya lazima, lakini pamoja na kwamba imesaidia kukuza mavuguvugu ya wananchi kinyume na sehemu nyingi— Palestina, Papua ya Magharibi, Sahara ya Magharibi na Tibet— mapambano hayo bado hayaeleweki.

Je, nini kinasababisha utofauti huu baina ya mifano hiii na mingine?

Mambo yaliyosababisha mavuguvugu haya na mengine kufanikiwa au la ni jambo ambalo watu makini wanaweza wasikubaliane kimtazamo.[1]  Kila hali ni ngumu sana kueleweka na kujaribu kuhusianisha sababu ni ngumu sana. Hoja ambazo mara nyingi nimekuwa nikizisikia kutoka kwa wanazuoni, waandishi wa habari, na wengine ni kwamba matukio haya na matokeo ya mavuguvugu haya na mengine ambayo kwa kiasi kikubwa ni ya amani yalisababishwa  na mifumo, hali na mazingira ya kipekee ambayo kila vuguvugu lilipitia katika uendeshaji wake.

Kwa mfano, kuna hoja kwamba mavuguvugu ya kudai haki kwa njia ya amani hufanikiwa tu kwenye jamii ambazo hasimu hayuko tayari  kutumia nguvu kupita kiasi. Wengine wanasema vigezo fulani vya kiuchumi (yaani itikadi ya kiuchumi, viwango vya kipato, mgawanyo wa mali, uwepo wa tabaka la kati) na viwango vya elimu ni msaada sana kwenye mavuguvugu yenye kuzaa matunda. Wengine wanadai kwamba mataifa makubwa na watawala wa kanda huonekana kuuzidi umuhimu wa viashiria vingine katika kuangalia matokeo ya vuguvugu. Idadi ya mifumo na hali mtu anaweza kutaja—yaani tofauti za kikabila, historia ya siasa na utamaduni, idadi ya watu, ukubwa wa eneo — ni nyingi, na ili kuwa na uhakika, mazingira mengi yanaweza kuhamasisha vuguvugu.

Kwa kufananisha sababu zzitokanazo na miundo na mazingira ni sababu zinazozingatia maarifa katika kusuluhisha migogoro kwenye vuguvugu, kile wanazuoni wanachoita “uwakala”.  Maarifa na uwakala ni mambo ambayo vuguvugu linaweza kudhibiti: hatua gani ya kimkakati vuguvugu linaweza kuchagua; lugha gani litumie ili kuwaleta watu pamoja na kuhakikisha lao moja; namna

linaweza kutengeneza shirikisho; wapi na kwa namna gani linaweza kukabiliana na hasimu wake; na maamuzi mengine lukuki katika kutumia nguvu ya umma.

Kwa mtazamo wangu, sababu hizi ambazo ni za kielimu zaidi huwa zinaangaliwa kiasi sana au zinapuuzwa na wale wanaojihusisha au wachambuzi wa mavuguvu ya amani. Kwanini iko hivyo, siyo lengo la makala haya, lakini sababu moja ni kwamba pengine watu wana wasiwasi au hawajui mazingira ambayo kitendo cha kudai haki kwa amani kinategemea—kwamba kwa kugeuziana kibao, nguvu inaweza kuruhusiwa kutumika tena na mahasimu katika kukabiliana na mavuvuguvu ya umma. Badala yake, wanahitimisha kwamba lazima kuwepo na sababu za nje au mazingira ya kustaajabia sana yaliyosababisha kutokea vuguvugu kama lilivyotokea.

Hata hivyo, tunaweza kuheshimu umuhimu wa miundo na mazingira katika kushawishi matukio na matokeo ya mavuguvugu ya amani bila kusahau umuhimu wa uwakala na maarifa. Kwakweli uwakala na maarifa huleta matokeo, na mara nyingine vimesaidia mavuguvugu kuzishinda, kuzipindua, au kuzibadili hali za kishindani.

Umuhimu, na mara nyingine kipaumbele cha maarifa na uwakala vinachukuliwa kama elimu ya kawaida kwenye fani nyingine kama biashara au namna ya kuwaza kijeshi. Kwanini mapambano ya amani yawe tofauti katika muktadha huu? Generali wa jeshi au Mkurugenzi wa shirika anaweza kucheka kama angeambiwa kwamba mkakati si kitu katika kuleta matokeo chanya kwenye majukumu yake. Kitabu matata *The Art of War (*yaani *Sanaa ya Vita)* cha Sun Tzu pengine kisingejulikana sana kama watu wangefikiri kwamba matokeo ya migomo na mazungumzo ya kujenga hoja yanatayarishwa mapema kwa kutegemea hali za kiuchumi.

Sasa tukirudi kwenye swali letu la msingi kwenye makala haya — ini husababisha mavuguvugu ya amani kufanikiwa? — tunaweza kuanza kupata majibu kwa kuangalia chaguzi za kimkakati na kile kimekuwa kikifanywa kwenye mavuvugu ya kihistoria. Kuna sababu nyingi zinazohusiana na uwakala na maarifa ambazo zinaweza kusababisha matokeo chanya ya vuguvugu, lakini (kwa ajili ya urahisi) kama tukichuja sababu kupata za muhimu zaidi, sababu tatu za mafanikio kwenye mavuguvugu ya amani ni: umoja, kuweka mipango, na maandamano ya amani.

## Umoja, kuweka mipango na maandamano ya amani

Kwa haraka haraka umuhimu wa sababu hizi unaweza kuwa wazi. Hata hivyo, undani wa sababu hizi na matokeo yake makuu hayaonekani mtu akiangalia mavuguvugu kwa kina. Kila mojawapo inahitaji ufafanuzi.

*Umoja* ni muhimu kwa sababu mavuguvugu ya amani hupata nguvu kutoka kwa wananchi kutoka secta mbalimbali za jamii. Kwa maneno: idadi ni kitu muhimu sana. Kadiri vuguvugu linavyokuwa na watu ndivyo uhalali wake, nguvu, na mbinu zinavyoongezeka. Hivyo basi, mavuguvugu yenye ushindi, huendelea kufikia makundi mapya kwa mfano wanaume kwa wanawake; vijana kwa wakubwa na wazee; waishio mijini na walio vijijini; walio wachache; waumini wa taasisi za kidini; wakulima, wafanyakazi, wafanya biashara, na mabingwa; matajiri, tabaka la kati, na wenye kipato kidogo; polisi, wanajeshi, na wanasheria, pamoja na makundi mengine.

Mavuguvugu yenye mafanikio huwafikia pia waungaji mkono wa mahasimu wao, wakijua kuwa moja ya mbinu bora kwenye nguvu ya umma kwenye kuwakutanisha watu ni uwezo wa kuwavutia wengine kubadili uungaji mkono au kupuuzia maagizo bila kujali vyeo. Kwa mfano, shughuli kusimama wakati wa vuguvugu la kupinga ubaguzi wa rangi Afrika Kusini lililotaka usuluhishi wa kitaifa liliungwa mkono na wengi na kuleta umoja kwa ajili ya mabadiliko, hata wazungu kadhaa waliokuwa wanaiunga mkono serikali ya kibaguzi waliigeuzia kibao.

Washiriki wa mavuguvu ya amani wanatakiwa pia kufanya maamuzi magumu juu ya mbinu gani zitumike kwenye mavuguvugu yao. *Kuweka mpango mkakati* ni jambo muhimu sana katika kufanikisha hili. Hata kama kuna sababu ya msingi au mambo yaliyofanywa na hasimu hayakubaliki, haiwezekani kuushinda ukandamizaji kwa kukurupuka tu katika kupambana, hata kama mambo hayo yamefanywa na hasimu kwa kiwango cha juu. Badala yake, mavuguvugu hupata nguvu pale tu mipango ya namna gani nguvu ya umma inaweza kutumika bila kukatizwa katizwa na kuungwa mkono na watu katika jamii ili kufanikisha malengo pangwa na kusudiwa. Kuamua mbinu gani zitumike na kwa mwendelezo upi; kuendeleza mawazo kwa ajili ya mabadiliko kwa kujikita kwenye malengo na manung'uniko ya watu ambao vuguvugu linalenga kuwasemea; kupanga watu gani mmoja mmoja au kwa makundi kuwalenga na kwa mbinu gani na kufikia malengo ya muda mfupi, wa kati na mrefu; kuweka mawasiliano mazuri ili kwamba kuwe na kukaa meza moja ili kuwe na shirikisho ni baadhi tu ya mambo ambayo mavuguvugu yanatakiwa wekea mikakati kwa mapana. Katika kufanya hayo lazima kuwe na uchambuzi jumuishi wa mazingira ambayo mapambano ya amani yanafanyikia. Kama sehemu ya mchakato wa kuweka mipango, mavuguvugu ya kweli hukusanya taarifa kwa njia rasmi au zisizo rasmi, huwasikiliza wananchi wa kawaida, na kujifanyia uchambuzi yenyewe, pia kwa ajili ya mahasimu wao na mtu wa tatu ambaye hajaamua kuingia miguu yote kwenye mgogoro huo.

Mwisho, mkakati hufanikiwa ikiwa tu umetekelezwa kwa nidhamu. Kushindwa kwenye vuguvugu la amani ni pale baadhi ya washiriki kushindwa kuwa na kudai haki kwa njia ya amani. Hivyo basi, maandamano ya amani — uwezo wa wananchi kuendelea kudai haki kwa njia ya amani, hata kama wanachokozwa — ni muhimu kuchochewa kwa washiriki. Kuna sababu za msingi kabisa katika hili. Matukio ya uvunjifu wa amani kupitia kwa washiriki wa vuguvugu yanaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa sana uhalali wa vuguvugu, na hivyo kumpa hasimu sababu za kuanza kamatakamata. Zaidi ya hilo, vuguvugu ambalo ni la amani muda wote lina nafasi kubwa zaidi ya kupata makundi mengi yenye msaada —ikiwa ni pamoja na hata waliokuwa wanamwunga mkono hasimu— kupitia mapambano.

Sababu kamili juu ya hili zinaweza kutengeneza kitabu, mafunzo juu ya nguvu ya umma ni muhimu sana na mafunzo ya mwendelezo bado yanapokea mwamko mkubwa. Kila vuguvugu linalojitokeza huongeza maarifa kwenye uelewa wa pamoja juu ya suala hili, ingawa bado kuna umuhimu wa kuona kwa mapana na kuendeleza aina hii ya matendo kisiasa na kijamii kwa kupitia sanaa na sayansi.

Hata hivyo, sababu hizi tatu —umoja, kuweka mipango, na maandamano ya amani — ni endelevu, na kwa mantiki hiyo hutoa muundo mzima ambao washiriki na waunga mkono wa mavuguvugu, pia watoa taarifa na wanaojifunza, wanaweza kuona kirahisi hali ya vuguvugu. Je, lina umoja? Je, lina mipango? Je, lina nidhamu? Matendo ya wale wanaotekeleza kanuni hizi

kwenye mapambano bila kutumia silaha wameshatengeneza njia ya kuelekea dunia yenye amani na haki. Kesho itafuata wale wanaoendelea kitumia kanuni hizo.

---

[1] Kwa faida ya makala haya, natoa maana ya mavuguvugu "yaliyofanikiwa" kama mavuguvugu ambayo yametekeleza malengo pangwa na mavuguvugu "yaliyoshindwa" ni yale ambayo yameshindwa kufikia malengo pangwa. Kuna suala la muda pia kwenye ufafanuzi huu. Vuguvugu lililofanikiwa hutimiza malengo tajwa (kwa mfano vuguvugu la Orange nchini Ukraine mwaka 2004) lakini changamoto kwenye kufanikisha vuguvugu miaka inayofuata zinaweza kusababisha kurudi nyuma (kwa taarifa zaidi juu ya kesi Ukraine, soma makala ya ya Novemba 17, 2010 "The struggle after people power wins" (yaani Mapambano baada ya ushindi wa nguvu ya umma) yaliyoandikwa na Olena Tregub na Oksana Shulyar na kuchapishwa kwenye Jukwaa la openDemocracy). Kwa upande mwingine, vuguvugu linaloshindwa kutimiza malengo yake (kwa mfano vuguvugu la kudai demokrasia nchini China la mwaka 1989) linaweza kusababisha madhara miaka inayofuata ikawa ndo sababu ya vuguvugu endelevu (kwa taarifa zaidi juu ya mfano wa China, soma makala ya Novemba 17, 2010 "Repression's Paradox in China" (yaani Sintofahamu ya kamatakamata China) yaliyoandikwa na Lester Kurtz na kuchapishwa kwenye Jukwaa la openDemocracy). Pamoja na kwamba si lazima kuliita vuguvugu kama "lililofanikiwa" au "lililoshindwa", matokeo haya mfuatano yanaweza kuwa na nguvu na ya muhimu kipekee.